

Maswali

1. Nani walikuwa adui wa Waisraeli?
2. Mbona Mungu hakukuwa akizuia Waisraeli kutoka kwa adui wao, Wafilisti?
3. Manoa na mkewe wiliita mwana wao eti nani?
4. Ni vitu vingapi viwili vyenye malaika aliambia Samsoni asivifanye?
5. Nini ilifanyika kwa Samsoni njiani alipokuwa akienda kuona mwanamke aliyempenda?
6. Baadaye Samsoni alipata nini kwa mwili wa simba?
7. Samsoni aliuliza wageni wake kitendawili gani?
8. Wageni walipata jibu la kitendawili namna gani?
9. Samsoni aliongoza Waisraeli kwa muda gani?
10. Waisraeli walifanya nini wakati Samsoni alikuwa akiwaongoza?

Majibu

1. Wafilisti walikuwa adui wa Waisraeli?
2. Watu walisahau Mungu na wakaanza kuabudu sanamu.
3. Waliita mwana wao eti Samsoni.
4. Lazima Samsoni asikunywe divai au asinyoe nywele.
5. Simba alishambulia Samsoni. Akaiuwa na mikono yake mitupu.
6. Samsoni alipata asali kwa mwili wa Simba.
7. "Kutoka kwa anayekula kulikuwa nyama. Kutoka kwa mwenye nguvu kukawa na kitu kitamu."
8. Wageni waliuliza mkewe Samsoni awambie jibu la kitendawili.
9. Samsoni aliongoza Waisraeli kwa miaka 20.
10. Waisraeli walipenda Mungu na kumtii wakati Samsoni aliwaongoza.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 2 Mwaka wa 2

52 Samsoni anauwa simba

Kwa Biblia

Waamuzi mlango wa 13 na 14

Kiini cha somo


Kuonyesha kwamba Mungu alijali watu wake wakati walimrudia kwa kumpende na kumtii.

Somo

Wafilisti walikuwa adui wa Waisraeli

Waisraeli walikuwa wakiishi kwa nchi ya Kanaani. Hii nchi walipewa na Mungu. Waisraeli walisahau Mungu tena. Walianza kuabudu sanamu. Hawakuuliza Mungu awasaidie.

Wafilisti walikuwa adui wa Waisraeli. Wafilisti walikuja na kushambulia Waisraeli. Walichukuwa baadhi ya miji ya Waisraeli. Waliharibu mazao na nyumba zao. Wafilisti waliwaletoa Waisraeli madhara mengi sana.



Baadaye Waisraeli walikumbuka vile Mungu alikuwa amewasaidia. Waliomba Mungu tena. Waliacha kuabudu sanamu. Mungu aliwasaidia.

Samsoni anazaliwa


Manoa na mkewe walikuwa wazee. Hawakukuwa na mtoto. Malaika aliwakujia siku moja. Malaika aliwambia kwamba watapata mwana. Hatakuwa mwana wa kawaida. Atakua ili aokoe watu wake, Waisraeli, kutoka kwa Wafilisti. Malaika aliwambia Manoa na mkewe kwamba huyo mwana lazima asikunywe divai. Lazima asinyoe nywele. Hii ilikuwa ishara kwamba yeye ni mtu wa Mungu asiye wa kawaida.

Manoa na mkewe walipata mtoto wa kiume. Jina lake walimuita Samsoni. Samsoni alikua akawa shujaa na wa nguvu. Samsoni alitii Mungu. Hakukunywa divai. Hakukata nywele zake. Mungu alimfanya Samsoni awe wa nguvu kwa sababu alimtii. Samsoni aliuwa Wafilisti wengi. Wafilisti walimuogopa Samsoni.

Samsoni anauwa simba

Samsoni alipenda mwanamke Mfilisti. Samsoni alienda kuuliza huyo mwanamke ili amwoe. Alipokuwa njiani, simba alitoka kwa kichaka na kumshambulia Samsoni. Samsoni alimua simba kwa mikono yake mitupu.

Baadaye Samsoni alienda kuoia yule mwanamke. Njiani alienda kuangalia mzoga wa huyo simba. Nyuki walikuwa wameingia na kukaa ndani ya mzoga. Ndani kulijaa asali. Samsoni alichukua kidogo na kula.



Samsoni anatega kitendawili

Samsoni alioa yule mwanamke Mfilisti. Kulikuwa na karamu ya harusi iliyochukua juma moja. Samsoni aliuliza wageni wake wategue kitendawili chake.

“Kutoka kwa anayekula kulikuwa na nyama,
Kutoka kwa mwenye nguvu kukawa na kitu kitamu.”

Samsoni alisema, “Mkinitegulia kitendawili changu kabla mwisho wa juma moja kuisha, nitampea mavazi 30 ya kitani na mavao mengine 30.”

Wageni walikubali.

Wageni hawakuweza hata kubaadisha kitendawili cha Samsoni. Waliambia mke wa Samsoni awasaidie kupata jibu. Kwa muda wote wa juma moja mkewe aliendelea kuuliza Samsoni amwambia jibu la kitendawili. Samsoni alichoka kuulizwa na mkewe amtegulie hicho kitendawili. Kwa siku ya mwisho ya juma, alimwambia jibu. Mkewe aliambia wageni. Wageni waliambia Samsoni, “Nini ni tamu kuliko asali? Nani ana nguvu kuliko simba?”

Samsoni alikasirika sana. Alisema, “Hamkujaribu kutegua nyinyi wenyewe kitendawili changu, mliteguwa kwa kudanganya mke wangu.” Samsoni alitoka nje na kuwaua Wafilisti 30. Alichukuwa shuka zao na nguo na akawapa wageni wake. Samsoni alienda nyumbani akiwa na ghadhabu kuu na akaacha mkewe. Baadaye mkewe alikufa.

Samsoni aliongoza Waisraeli kwa miaka ishirini. Aliwaokoa kutoka kwa ukatili na kushambuliwa na Wafilisti. Waisraeli walipenda Mungu na kumtii kwa mda wote Samsoni aliwaongoza.